JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# MAGAZETINI WIKI HII

Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA. Simu: +255 26 2310021 Barua pepe: km@sheria.go.tz

**HabariLeo 08/02/2023 U.k 18**




Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro akikata utepe kuzindua rasmi kitabu cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara katika sekta ya sheria katika hafla iliyofanyika jana mjini Dodoma. Wengine ni aliyekuwa Waziri wa wizara hiyo, Profesa Palamagamba Kabudi (wa pili kushoto), Kaimu Katibu Mkuu wizara hiyo, Neema Mwanga (kulia) na aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Sifuni Mchome. (Picha na Iddy Mwema).

# Wananchi wapoteza imani na taasisi za haki jinai

**Dar es Salaam**
**Na REHEMA MAIGALA**

MWENYEKITI wa Tume ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, Jaji Mkuu Mstaafu Othman Chande, amesema kuna mmomonyoko na upungufu wa imani kwa Watanzania katika taasisi zinazojishughulisha na haki jinai.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika kikao cha kupokea maoni kwa taasisi, Jaji Chande alisema malalamiko hayo yamemsababisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuunda tume hiyo iliyozinduliwa Januari 31 mwaka huu.

Alisema tume hiyo itashughulika na taasisi tano za haki jinai ambazo ni Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Jeshi la Magereza, Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) na Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Serikali (DPP).

"Hizo ndizo zinazozalisha manung'uniko kwa wananchi, hivyo tutashirikiana nao kuondoa changamoto hizo kwa wananchi. Tutakuwa tunafanya kazi kwa vitendo, tutawatembelea mahabusu kusikiliza maoni yao lengo ikiwa ni kuondoa msongamano ndani ya magereza," alisema.

Pia, alieleza kuwa tume hiyo ina majukumu mawili katika utekelezaji wake wa kazi ambayo ni kufanya tathimini ya mfumo wa haki jinai katika kuilinda jamii na haki zao pamoja na kudhibiti sheria na uhalifu.

"Lengo la Rais Dk. Samia katika tume hiyo ni kufanya maboresho ya haki jinai katika kuongeza weledi ili kutoa huduma bora kwa watu wote," alisema.

Jaji Chande alisema katika utekelezaji huo wa tume haki jinai, wataifikia mikoa 14 na wilaya 30 kwa ajili ya kukusanya maoni kutoka katika taasisi hizo na zile ambazo zipo katika mifumo ya haki jinai.

**Uhuru 10/02/2023 U.k 16**

# Samia atoa maagizo vyeti vya kuzaliwa

Na Mwandishi Maalumu

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano na wale walio katika taasisi za elimu wawe wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa ifikapo mwaka 2025.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro pia amesema amepokea maelekezo kutoka kwa Rais Samia kuwa watu wazima wawekewe mikakati ili ifikapo mwaka 2030 kila mwananchi awe na cheti cha kuzaliwa.

Dk Ndumbaro alisema ni lazima usajili ufungamanishwe na taasisi za elimu ili wakati wa usajili wa kujiunga na elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya juu wote wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa wapate fursa kupitia kambi maalumu ya usajili.

Alisema hayo jijini Dodoma wakati akizindua Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Dk Ndumbaro alisema usajili wa matukio muhimu ya binadamu ni nyenzo muhimu ya kuipatia serikali takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo na usalama wa nchi.

"Natoa maelekezo kwa RITA kuanzia sasa usajili ufanyike kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zote za serikali na watu binafsi, kwenye taasisi za elimu, kuanzia shule za awali, msingi, sekondari na vyuo mbalimbali lengo likiwa kuwafikia wananchi wengi zaidi," alisema.

Dk Ndumbaro aliiagiza bodi hiyo ya ushauri iishauri wizara kuhusu mambo ya kisera na utekelezaji wa majukumu ya RITA ili kuisaidia serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Alisema bodi hiyo imeundwa kwa mujibu wa sheria hivyo wajumbe wafanye kazi kwa uadilifu na weledi kwa maslahi ya nchi kulingana na sheria na kanuni husika.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk Amina Msengwa alisema watashirikiana na wizara na menejimenti ya RITA kwa kusimamia malengo na mikakati kwa kuwekeza zaidi katika mifumo ya kisasa ya utoaji wa huduma bora kidijiti.

Wajumbe wengine wa bodi hiyo ni Angela Anatory ambaye ni katibu, Profesa Abel Kinyondo, Erick Kitali, Theresia Mganga, Peter Mwambuja na Lucy Dinganyeki.

# Rais Samia aagiza Rita itoe vyeti kabla 2030

**Bakari Kiango**, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Rais Samia Suluhu Hassan, ameigiza Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (Rita), ihakikishe watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano na waliopo katika taasisi za elimu wasajiliwe na wapewe vyeti vya kuzaliwa ifikapo mwaka 2025.

Taarifa iliyotolewa jana Rita kwa vyombo vya habari, ilieleza kuwa maelekezo hayo yalisomwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro wakati akizindua bodi ya ushauri ya wizara kwa Rita.

Dk Ndumbaro alisema Rais Samia ameagiza Rita ihakikishe inaweka mkakati wa kuwasajili watu wazima na kuwapa vyeti vya kuzaliwa ifikapo mwaka 2030. Dk Ndumbaro alisema lazima usajili ufungamanishwe na taasisi za elimu ili wakati wa kujiunga na elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya juu wale wote wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa wapate fursa kupitia kambi maalum ya usajili zitakazoanzishwa katika maeneo yao.

Katika maelezo yake, Dk Ndumbaro alisema usajili wa matukio muhimu ya binadamu ni nyenzo muhimu ya kuipatia Serekali takwimu muhimu katika kupanga mipango ya maendeleo na usalama wa nchi hivyo ni muhimu mchakato huo ukafanyika sasa.

"Niwaagize Rita kuanzia sasa usajili ufanyike kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zote za Serikali na watu binafsi, kwenye taasisi za elimu, kuanzia shule za awali, msingi, sekondari na vyuo mbalimbali kengo likiwa kuwafikia wananchi wengi zaidi,"alisema Dk Ndumbaro.

**AHADI YA BODI**

**Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk Amina Msengwa alisema watahakikisha wanafanya kazi kwa pamoja na wizara na menejimenti ya Rita kusimamia malengo na mikakati itakayosaidia kuwekeza zaidi katika mifumo ya kisasa ya utoaji wa huduma bora Kidigitali**

**Wajumbe wa bodi hiyo ni Angela Anatory (Katibu), Profesa Abel Kinyondo, Erick Kitali, Theresia Mganga, Peter Mwambuja na Lucy Dinganyeki.**

# Tume ya Haki Jinai kutembelea mikoa 14, wilaya 30

**Na Aveline Kitomary**

TUME ya Haki Jinai imesema itatembelea mikoa 14 na wilaya 30 nchini kukusanya mapendekezo kuhusu taasisi zilizokusudiwa, na ripoti itawasilishwa Mei 2, mwaka huu.

Tume hiyo pia imesema itashiriki kukusanya maoni ya wananchi kwa kupitia njia mbalimbali kama vile mitandao ya kijamii kama Facebook, Twitter, Instagram, WhatsApp, mahojiano ya ana kwa ana na kwa njia ya kupiga simu kwa siku 120 walizopewa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman alisema wana majukumu mawili likiwamo la kufanya tathmini ya mfumo wa haki jinai.

"Na madhumuni hayo yote ni kulinda jamii na mali zao, kudhibiti sheria, kudhibiti wahalifu, kurekebisha walioti wa hatiani na katika hilo tunaangalia mfumo mzima wa haki jinai," alieleza mwenyekiti huyo.

Alisema katika mchakato wa utendaji kazi wa tume hiyo watatathmini taasisi tano za haki jinai; Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Jeshi la Magereza, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya (DCEA).

"Lakini pia kuna taasisi ambazo ziko zinahusika pia kama Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ya Misitu, Mahakama ya Tanzania pia kwani zinatumia mfumo mmoja hapo taasisi ni tofauti," alisema.

Alisema lengo la Rais Samia Suluhu Hassan ni kuboresha haki jinai ili kutoa huduma bora kwa wananchi huku haki ikitendeka ili kukidhi matakwa ya Watanzania.

"Tunamshukuru Rais kwa imani aliyonayo, tumeanza kazi tarehe sita, tumeshaonana na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Mkuu wa Jeshi la Magereza, wakurugenzi wa Mashtaka Tanzania na Zanzibar, Kamishna wa Dawa za Kulevya kutoka Zanzibar," alieleza.

Alimshukuru Rais Samia kwa kulipa uzito haki jinai kwani kuna upungufu wa imani ya Watanzania kwa mamlaka za utoaji haki na mfumo wenyewe.

Alibainisha kuwa uboreshaji wa taasisi hizo utaleta huduma bora zenye usawa kwa Watanzania.

Aliongeza kuwa watafanya mahojiano na taasisi mbalimb[...] kuanzia ngazi za juu hadi chin[...] ikiwamo kutembelea magerez[...] kuzungumza na wafungwa, a[...] za kiraia, makundi ya wanaw[...] taasisi za haki za binadamu na zingine.

"Madhumuni ya tume ni kutathmini mfumo wa haki ji[...] kutathmini utendaji wa taasisi[...] sio wa mtu mmoja mmoja pia naalika mtu yeyote kutoa mao[...] alisema.

"Waje watupe maoni na na[...] ya kutatua mfano ucheleweshe[...] wa kesi tunatatua vipi. Mfano [...]ereza ambayo yana msongam[...] tutatue vipi, tutawatengeneza[...] wafungwa waje kuishi katika [...] bila kurudia makosa yako, ku[...] nidhamu," alisema.

# Bunge labaini changamoto miswad[...]

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

BUNGE limebaini kuwa uandishi wa sheria katika lugha ya Kiswahili peke yake una changamoto.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Dk Joseph Mhagama alisema moja kati ya changamoto hizo ni uchache wa misamiati na istilahi za kisheria katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuleta ugumu katika tafsiri.

Dk Mhagama alisema hayo bungeni Dodoma jana wakati akiwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha kuanzia Februari mwaka jana hadi Januari mwaka huu.

Kamati iliipongeza serikali kwa kutekeleza ushauri wa Bunge wa kuwasilisha miswada kwa Kiswahili lakini ikasema sheria zilizoandikwa kwa lugha hiyo peke yake zinaweza kuleta changamoto kwa Mahakama katika kufikia uamuzi hasa kwa kuzingatia kwamba mfumo wa sheria wa nchi unazingatia misingi ya Jumuiya ya Madola.

"Bila kuathiri nia njema ya serikali katika kutekeleza maoni ya Bunge kuhusu lugha ya uandishi wa sheria kuwa Kiswahili, kamati imetafakari uwezekano wa kufanyika

marekebisho tena ili sasa miswada ya sheria iwasilishwe bungeni kwa lugha zote mbili, yaani Kiingereza na Kiswahili," alisema Dk Mhagama.

Alisema lengo la mapendekezo hayo ni kuwapa wabunge wigo mpana wa kuelewa kwa kina masharti na mapendekezo ya miswada husika.

Dk Mhagama aliwaeleza wabunge kuwa katika uchambuzi kamati ilifanya rejea katika nchi nyingine za Jumuiya ya Madola ili kupata uzoefu wa namna nchi hizo zinavyotumia lugha ya Kiingereza na lugha za asili ya nchi hizo katika uandishi wa miswada.

Alisema katika nchi ya India Bunge la Juu la India (Rajya Sabha) limeweka utaratibu kwa uamuzi wa Bunge kwamba, muswada wowote unapowasilishwa bungeni ni lazima uwe katika nakala ya Lugha ya Kiingereza na nakala katika Lugha ya Kihindi.

"Msimamo huu unaweza kulisaidia Bunge letu na serikali kwa ujumla kutafakari kwa pamoja ili endapo kutakuwa na ulazima, basi marekebisho ya sheria yafanyike ili kuakisi msimamo kuhusu lugha rasmi ya uandishi wa sheria za nchi yetu," alisema Dk Mhagama.

# Bunge latoa siku 60 marekebisho sheria ndogo

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

BUNGE limeelezwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zina dosari na limetoa siku 60 zirekebishwe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Dk Jasson Rweikiza alisema Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi zirekebishe sheria ndogo hizo ndani ya siku 60 ili kuondoa dosari hiyo.

Dk Rweikiza alisema hayo bungeni Dodoma jana wakati akiwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati hiyo kwa kipindi cha Februari mwaka jana hadi Januari mwaka huu.

"Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizokutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ndani ya sitini kuanzia leo (jana) ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo," alisema.

Pia Dk Rweikiza alisema Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo (jana), ili kuendana na uhalisia na kurahisisha utekelezaji wake.

"Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze maazimio hayo ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023," alisema.



Dk Rweikiza aliwaeleza wabunge kuwa sheria ndogo 13 zina masharti yanayokinzana na Katiba na nyingine 10 zina masharti yanayokinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Alilieleza Bunge kuwa sheria ndogo 27 zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi.

"Makosa hayo nia kama vile kutorejea vifungu sahihi, kurejea vifungu ambavyo havipo, kutokukamilika kwa sheria ndogo kwa kutokuwepo kwa baadhi ya vipengele muhimu vya kisheria ili kukamilisha sheria husika," alisema Dk Rweikiza.

Alisema sheria ndogo 12 zinaweka masharti yasiyo na uhalisia ambayo yataleta changamoto katika utekelezaji wake na sheria ndogo 15 zina makosa ya maudhui ya majedwali kutofautiana na vifungu vinavyoyaanzisha au makosa ya kutokukamilika kwa majedwali au kuanzishwa kwa majedwali yasiyokuwepo ama kukosekana kwa majedwali.

# Mchakato kupitia sheria kandamizi waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila, ili kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane kwenye mirathi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali inawasaidiaje wajane ili kuondoa mila na desturi potofu zinazo mkandamiza mwanamke kwenye mirathi.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema serikali inatambua uwepo wa wajane na katika kulinda haki zao kwa kutunga sheria mbalimbali na kanuni za kulinda haki za wanawake katika suala zima la mirathi.

"Suala la mila na desturi potofu ni eneo ambalo serikali imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila, ili kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane katika suala la mirathi. Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu sheria ya mirathi hususan umuhimu wa kuandika wosia katika kuondoa changamoto zinazotokana na mila na desturi potofu," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuajiri wanasheria, ili kusaidia kutoa elimu ngazi ya kata kutoa elimu ya mirathi.

"Inasikitisha na kuona huzuni wanawake wajane wamejikunja hawajui hatima yao kwasababu wanadhurumiwa haki yao ya mirathi serikali ina mpango gani wa kuleta sheria ili kuondokana na tatizo hili," alisema.

Akijibu maswali hayo, Pinda alisema mtu anapopewa nafasi ya kuwa msimamizi wa mirathi anajiona ni mrithi wakati yeye sio mrithi anatakiwa kusimamia warithi kupata haki zao.

"Kwa sasa mtu akipewa nafasi anaanza kujinufaisha mwenyewe huyu ni mrithi anatakiwa kushtakiwa, kinamama wananyanyasika kutokana na mashemeji waliopewa jukumu la kusimamia mirathi kula mali za marehemu," alisema.

Aidha, alisema kuna mila zinafanya msimamizi wa mirathi kuwa na sauti kwa asilimia 100, lakini hilo halipo kisheria.

# Sheria za kimila kufanyiwa mapitio kuondoa ukandamizaji

WIZARA ya Katiba na Sheria, imeanzisha mchakato wa kufanya mapitio ya sheria za kimila kwa dhumuni la kuondoa ukandamizaji kwa wajane katika suala la mirathi.

Hayo yalisemwa jijini hapa bungeni jana na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Godfrey Pinda, wakati akijibu swali la Mbunge Viti Maalumu (CCM), Suma Fyandomo.

Mbunge huyo alitaka kujua serikali inawasaidiaje wajane kuondoa mila na desturi potofu zinazomkandamiza mwanamke katika suala la mirathi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Pinda alisema serikali inatambua uwepo wa wajane na katika kulinda haki zao ndio

> **"Suala la mila na desturi potofu ni eneo ambalo serikali imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane katika mirathi.**
>
> Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Godfrey Pinda.

maana imetunga sheria na kanuni za kulinda haki za wanawake katika suala la mirathi.

"Suala la mila na desturi potofu ni eneo ambalo serikali imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane katika mirathi. Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu sheria ya mirathi hususan umuhimu wa kuandika wosia kuondoa changamoto zinazotokana na mila na desturi potofu," alisema.